MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU

Tarehe 30 Disemba 2007, baada ya kutangazwa matokeo ya kura za rais, vurugu za utumiaji nguvu zilizuka kwenye maeneo kadha nchini Kenya huku kukiwa na madai kwamba Tume ya Uchaguzi ya Kenya (ECK) ilikuwa imetumia udanganyifu kwenye uchaguzi wa rais. Vurugu za utumiaji nguvu za hapa na pale ziliendelea kwa majuma kadha na kusabisha vifo na uharibifu wa mali kwa maelfu ya Wakenya. Jopo la Waafrika Maarufu likifadhiliwa na Umoja wa Afrika na kuongozwa na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa Kofi Anan lilisaidia kuleta makubaliano ambayo yaliwezesha kuundwa serikali ya mseto baina ya vyama vikuu vya kisiasa na pia kupatikana kujitolewa kwa pamoja kwa lengo la marekebisho ya katiba. Makubaliano hayo yalikuwa ni pamoja na kuteuliwa tume mbili. Tume mojawapo ilikuwa ya kuchunguza vurugu za utumiaji nguvu na ya pili - Tume Huru ya Uchunguzi, (IREC) - ikapewa jukumu la kuchunguza uchaguzi wa Kenya wa 2007 kutoka mikabala mbalimbali.

Kwa kuzingatia maagizo yake ya kazi, IREC sasa inawasilisha mambo iliyogundua na pia mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa muundo wa kisheria wa kuendesha uchaguzi nchini Kenya, mfumo wa mpangilio, muundo na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi ya Kenya (ECK) na mipango na uendeshaji wa upigaji kura wa 2007. Ripoti hiyo ambayo hasa inachunguza uadilifu wa harakati zote za upigaji kura kuanzia kusajilishwa wapiga kura na kuteuliwa kwa wagombeaji viti, kupitia kupiga, kuhesabu, kusafirisha na kujumlisha kura hadi usuluhishaji wa kutoelewana na taratibu za baada ya uchaguzi, inahusu wajibu wa vyama vya kisiasa, wachunguzi wa uchaguzi, vyombo vya

habari, makundi ya kiraia na umma kwa jumla, na inatoa maoni juu uhuru, uwezo na ubora wa kazi ya ECK.

Mambo Muhimu Yaliyogunduliwa na Tume

Mfumo wa Kenya wa kikatiba na kisheria kuhusiana na uchaguzi una udhaifu na ulegevu wa aina mbalimbali ambao unadhoofisha uwezo wake wa kutenda kazi. Sheria zinazohusika zinahitaji marekebisho makubwa na ya dharura, ikiwa ni pamoja na kuletwa pamoja kwa sheria hizo.

Utaratibu mzima wa kusimamia uchaguzi unahitaji marekebisho.

Wakati wa kufanya maandalizi na kuendesha uchaguzi wa 2007, ECK haikuwa na uhuru unaohitajika, uwezo wa kikazi na utendaji kazi mzuri kutokana na udhaifu katika mpangilio wa tume, muundo wake na mifumo yake ya usimamizi.
Kukubalika kwa ECK na imani ya umma kuhusu uwezo wa kitaaluma wa wanatume na wafanyikazi wake wengine ni mambo ambayo yameharibiwa kwa kiwango kikubwa kwa kadri isiyoweza kurekebishwa. Tume hiyo haina utendaji kazi mzuri na haiwezi kutekeleza wajibu wake kama inavyohitajika.

Uendeshaji wa utaratibu wa uchaguzi ulitatizwa na mienendo ya washiriki wengi hasa vyama vya kisiasa na vyombo vya habari. Washiriki hawa na wengineo pia walichafua mazingara ya uchaguzi.

Kulikuwa na makosa mengi kwenye usajilishaji wa wapiga kura jambo ambalo liliharibu imani kuhusu uchaguzi wa 2007 hata kabla ya upigaji kura kuanza.

- Takriban thuluthi moja ya waliostahili kupiga kura hasa miongoni mwa wanawake na vijana haikusajilishwa
- Usajilishaji ulishirikisha majina ya watu milioni moja na laki mbili waliofariki.

Makosa makubwa sana kuhusiana na mipaka ya maeneo bunge yalitatiza ukubalifu wa utaratibu wa uchaguzi hata kabla ya upigaji kura kuanza.

Upigaji kura ulifanywa vibaya. Kulikuwa na utoaji rushwa kwa wingi, ununuaji kura, vitisho na kuongezwa kura katika masanduku ya kura.

Jambo hilo lilifuatwa na makosa makubwa katika upangaji wa habari za kura, kuzisafirisha na kujumlisha kura. Kwa hivyo, utaratibu wa kupiga kura haukufaulu kutona na ukosefu wa kiwango cha kutosha kuhusiana na mipango, uajiri wa wafanyikazi na utoaji mafunzo kwao, mawasiliano na umma, na utatuzi wa kutoelewana.

Ukubalifu wa utaratibu wa kupiga kura na kuaminika kwa matokeo ya uchaguzi kulitatizwa pakubwa sana na makosa haya hivi kwamba haijalishi kama kwa hakika kulikuwa na udanganyika kwenye kituo cha kitaifa cha kujumlisha kura. Matokeo ya uchaguzi yana udhaifu usioweza kurekebishwa.

Mapendekezo Makuu

Washiriki wote wa kisiasa nchini Kenya wanapaswa kutambua kwamba uchaguzi uliokuwa na makosa kimsingi na ambao ulifuatwa na vurugu za umma za utumiaji nguvu ni jambo litaloendelea kuonekana nchini mwao isipokuwa kufannywe juhudi thabiti na kuwe na kujijtolea vilivyo kuhusiana na uadilifu wa uchaguzi miongoni mwa Wakenya wote.

Rekebisheni ECK kwa kiwango kikubwa sana au muunde taasisi mpya ya kusimamia uchaguzi (EMB) ikiwa na jina, sura na maadili mapya ya kitaifa na ambayo imejitolea kuwa na kiwango cha juu kabisa cha ubora wa usimamizi ili kuleta kuaminika uchaguzi. Taasisi hiyo iwe na halmashauri ya watu wachache ya kuunda sera na kuangalia shughuli na iwe imeteuliwa kwa namna wazi na isiyobagua na ifanye kazi na ofisi ya kitaaluma yenye muundo mzuri.

Undeni, mtumie na mhifadhi hatua zinazofaa za kiusimamizi, kiundaji sheria na kisiasa ili kuwezesha taasisi ya uchaguzi iliyorekebishwa au taasisi mpya kuanzisha, kueneza miongoni mwa watu na kudumisha kujitolea kwa kitaifa kwa uaminifu wa uchaguzi na heshima kwa haki ya kupiga kura ya wananchi wa Kenya.

Patieni EMB uwezo kupitia hatua za kiusimamizi, kiundaji sheria na za kisiasa ili iweze kutekeleza kwa namna nzuri shughuli muhimu iliyopewa chini ya sehemu 42 na 42A za katiba (uwekaji mipaka na uendeshaji wa uchaguzi na shughuli nyingine zinazohusika).

Kuweni na mfumo mpya wa kusajilisha.

Afikianeni (kama sehemu ya utaratibu wa marekebisho ya katiba) kuhusu mfumo wa uchaguzi ambao utatia kikomo mjadala unaoendelea kuhusu mfumo mpya wa uchaguzi nchini Kenya.

Chagueni na mtekeleze marekebisho yanayofaa ya kikatiba na kisheria ili kutimiza mapendekezo yoyote yanayokubalika ya IREC.

Maoni ya Wachache

Wanatume wawili walikuwa na maoni tofauti kwa baadhi ya mambo yaliyogunduliwa na tume hii na kuandikwa katika Sura ya 6. Maoni yao yamewasilishwa kwa maandishi ya mlazo mwishoni mwa kila aya inayohusika.